(vii) Matini ya Hadithi za Mtume (s.a.w) maana yake ni

A mapokezi ya Hadithi zaidi ya moja
B ufafanuzi wa Qur'an tukufu
C kigezo cha usahihi wa Isnad
D kauli au matendo ya Mtume (s.a.w)
E kauli na matendo ya Muhadithina.

(viii) Katika kipindi cha Maswahaba (Tabii-Tabiina), wanazuoni walioifanya elimu ya Hadithi kuwa fani miongoni mwa fani za elimu ya Kiislamu ni

A Suyut na Ibn Hajar Asqalah
B Bukhar na Muslim
C Ahmad bin Hambal na Malik bin Anas
D Umar bin Abdul-Aziz na Suyut
E Tabaran na Al-Qutmiy

(ix) Katika mwaka wa 11 hadi 101 AH matatizo mengi yalitatuliwa kwa hukumu zilizotokana na

A maamuzi ya shura
B sharia za Kiislamu
C wataalamu wa Bani Umayah
D sharia za mahakama zilizotungwa na maswahaba
E Hadithi zilizohifadhiwa na maswahaba

(x) Miongoni mwa mambo muhimu ambayo yanatia nguvu usahihi wa Hadithi ni

A ushiriki wa mpokezi wa jihadi
B umri wa mpokezi
C uzalendo wa mpokezi
D imani ya mpokezi
E udhibitifu wa mpokezi.

CS17PREP



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

## SEHEMU B (Alama 15)
## QUR'AN

2. Oanisha maudhui ya Qur'an yaliyopo katika **Orodha A** na Sura za Qur'an zilizopo katika **Orodha B**. Andika herufi ya jibu sahihi kutoka Orodha B pembeni ya namba kutoka orodha A katika kijitabu chako cha kujibia.

| Orodha A | | Orodha B | |
|---|---|---|---|
| (i) | Sura nzima ya mwisho kushushwa kwa Mtume (s.a.w). | A | Al-Alaq |
| (ii) | Aya tano zilizofuatana zikiwahimiza wanadamu juu ya swala la kujielimisha. | B | Al-Falaq |
| (iii) | Allah (s.w) alionesha kuwepo kwake na uwezo wake pale alipomhilikisha Abrah na jeshi lake. | C | Al-Fatihah |
| (iv) | Qur'an ilianza kushushwa katika usiku wenye cheo. | D | Al-Baqara |
| (v) | Sura ndefu kuliko sura zote katika Qur'an. | E | Al-Lahab |
| (vi) | Ili mwanadamu apate kufuzu hapa duniani na Akhera hana budi kuchunga muda. | F | Al-Kafiruun |
| (vii) | Sura inayojulikana kwa jina la Ummul-Kitaab. | G | Al-Imraan |
| (viii) | Mwanadamu ameghafilika na lengo na hadhi yake hapa ulimwenguni na kupupia wingi wa mali, wake na watoto. | H | Al-Qadr |
| (ix) | Qur'an ilishushwa kwa lengo la kuwaongoza wanadamu. | I | Al-Asr |
| (x) | Tutakusomesha (tutakusomea) wala hutasahau. Ila akipenda Mwenyezi Mungu. | J | Al-Aala: 6-7 |
| (xi) | Tumuombe Allah (s.w) mahitaji yetu mbalimbali kwa kutanguliza sifa zake tukufu. | K | Al-Ikhlas na Al-Falaq |
| (xii) | Al-Muawwidhatain ni jina la pamoja la Sura mbili. | L | Al-Baqara: 2 |
| (xiii) | Makuraysh walimtaka Mtume (s.a.w) ashirikiane nao katika ibada. | M | At-Takaathur |
| (xiv) | Ardhi itatoa maelezo ya mambo yote yaliyotokea duniani. | N | Al-Fatihah: 2-5 |
| (xv) | Miongoni mwa miujiza ya Qur'an ni kutosilimu kwa ami yake Mtume (s.a.w) mpaka kufa kwake. | O | Quraysh |
| | | P | An-Nasr |
| | | Q | Al-Fiil |
| | | R | Al-kauthar |
| | | S | An-Naas na Al-Falaq |
| | | T | Az-Zil-Zal |

CS17PREP



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

## SEHEMU D (Alama 30)
## FIQH

4. Jibu maswali yafuatayo kwa kifupi kwa **kuandika majibu** katika kijitabu chako cha kujibia.

(a) Ili kuthibitisha kuingia katika Uislamu mtu hutakiwa kufanya jambo gani? Taja jambo hilo.

(b) Nguzo za tayamam ni nne; taja nguzo mbili tu kati ya hizo.

(c) Orodhesha swala ambazo haziingii katika tahfifu ya kupunguza rakaa.

(d) Taja mambo mawili ambayo yakifanywa ibada ya Umra hukamilika.

(e) Bainisha nisaab ya ng'ombe na kiasi cha kutoa.

(f) Ainisha sifa mbili za mashahidi wanaopaswa kushuhudia ndoa ya Kiislamu.

(g) Orodhesha mambo mawili yanayoharibu funga (swaumu) ya mtu.

(h) Tofautisha kati ya mfumo wa uchumi wa Kiislamu na wa Kijahili kuhusu dhana ya bidhaa.

(i) Elezea tofauti iliyopo kati ya adhabu ya mlevi na ya mzinifu.

(j) Toa maelezo mafupi kuonesha jinsi msafiri alivyorahisishiwa swala.

(k) Taja sifa mbili za Waislamu wanaolazimika kufunga mwezi wa Ramadhani.

(l) Orodhesha mambo mawili yanayomzuia mtu kurithi mali.

(m) Bainisha hukumu ya mwanamke aliyeachwa na mume mara baada ya kufunga ndoa lakini hawajafanya tendo la ndoa.

(n) Andika tafsiri ya aya inayoonesha lengo la kutoa zaka.

(o) Bainisha nafasi ya Mwenyezi Mungu na mwanadamu katika falsafa ya umilikaji mali kwa mtazamo wa Uislamu.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

## SEHEMU E (Alama 30)
## TAREKH

5. Chagua **neno** au **kifungu cha maneno** (i) – (xxx) ili ukamilishe sentensi (a) – (o) kwa kuandika majibu sahihi tu katika kijitabu chako cha kujibia. Maneno au vifungu vya maneno vinaweza kutumika zaidi ya mara moja.

| | | | |
|---|---|---|---|
| (i) | Mkweli | (xvi) | Hijjatul-wadai |
| (ii) | Kiuchumi | (xvii) | Kudhihakiwa |
| (iii) | Wayahudi | (xviii) | Ali na Muawiya |
| (iv) | Qur'an | (xix) | Ugonjwa |
| (v) | Ummul-Qura | (xx) | Umayya bin Khalaf |
| (vi) | Sarah | (xxi) | Nyani |
| (vii) | Jaffar bin Abuu Talib | (xxii) | Mwaminifu |
| (viii) | Maovu | (xxiii) | Kielimu |
| (ix) | Hifadhi | (xxiv) | Aqaba |
| (x) | Kupigania uhuru | (xxv) | Nashrah |
| (xi) | Al-balad-amin | (xxvi) | Habasha |
| (xii) | Adam na Hawa | (xxvii) | Hajir |
| (xiii) | Mhabeshi | (xxviii) | Kisiasa |
| (xiv) | Kudharauliwa | (xxix) | Wakristo |
| (xv) | Abuubakar na Omar | (xxx) | Sunnah |

**Maswali**

(a) Mambo mawili maarufu yanayoonesha kuwa Mitume hawaathiriwi na mazingira katika maisha yao kabla ya kupewa utume kwa Mtume (s.a.w) ni __________ na __________.

(b) Makafiri wa Makka walimpinga Mtume (s.a.w) na utume wake kwa sababu za __________ na __________.

(c) Wapinzani wa dola ya Kiislamu walikuwa Makafiri wa Kikureish na wasaidizi wao, wanafiki, __________ na __________.

(d) Serikali huwa ya Kiislamu pale inapoendeshwa kwa misingi ya __________ na __________.

(e) Kwa mtazamo wa Uislamu, asili ya mwanadamu si __________ ; wala hadhi yake hapa ulimwenguni si sawa na ile ya mnyama kwani Qur'an inatufundisha kuwa binadamu wote ni watoto wa __________.

(f) Bilal alikuwa __________ na mtumwa wa __________ ambaye alikuwa adui mkubwa wa Uislamu.

(g) Miezi miwili baada ya __________ Mtume (s.a.w) alishikwa na __________.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

(h) Kikundi cha Waislamu kiitwacho Khawarij walikubali mamlaka au ukhalifa wa __________ tu hawakumkubali __________.

(i) Miongoni mwa mateso ya kisaikolojia aliyoyapata Nabii Nuhu (a.s) kutoka kwa wapinzani wa ujumbe wa Mwenyezi Mungu ni __________ na __________.

(j) Wake wa Mtume Ibrahim (a.s) walikuwa ni mama __________ na __________.

(k) Mzigo mzito uliomvunja Mtume (s.a.w) unaotajwa katika sura __________ ni __________ yaliyodumu kwa muda mrefu.

(l) Kiongozi wa Hijra ya mwanzo kuelekea __________ alikuwa ni __________.

(m) Mikataba ya __________ ilisaidia sana katika kumhakikishia Mtume (s.a.w) kupata __________ kule Madina.

(n) Waislamu wa Tanganyika walikuwa mstari wa mbele katika __________ kutokana na kunyanyaswa kwao __________.

(o) Kutokana na utukufu wake mji wa Makka pia umeitwa katika Qur'an kwa jina la __________ yaani mama wa mji (Qur'an 42:7) na pia umeitwa __________ yaani mji wa amani (Qur'an 95:3).



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

Scanned by CamScanner